# Tofauti baina ya Vivumishi na Vibainishi katika Lugha ya Kiswahili

Zabron T. Philipo


## Ikisiri

Nia ya makala hii ni kuonyesha tofauti ya dhana 'kivumishi' na 'kibainishi' katika lugha ya Kiswahili. Wanaisimu wengi, kwa kutumia mtazamo wa kimapokeo, wamekuwa wakichanganya dhana hizi mbili katika lugha hii ambapo vibainishi vimekuwa vikiwekwa kwenye 'kapu' moja na vivumishi. Kutokana na kuwapo kwa utata huo, makala hii inazitalii dhana hizi mbili ili kujaribu kuondoa au kupunguza utata unaowakabili wanaisimu katika kuzipambanua dhana hizi katika lugha ya Kiswahili. Mbinu ya udurusu wa nyaraka ilitumika kupata data za makala hii[1]. Mtazamo wa kisasa katika kuainisha tofauti baina ya vivumishi na vibainishi ulitumika. Mtazamo huu unasisitiza kutumia kigezo cha kisintaksia kupambanua aina hizi za maneno kwa kuzingatia: mosi, *mtawanyiko* wake, pili, *dhima kisarufi*, na tatu, *mnyambuliko* wa aina hizi za maneno. Aidha, makala hii inapendekeza vigezo na namna nyingine za kuainisha vibainishi na vivumishi katika lugha ya Kiswahili.


## 1.0 Utangulizi

Makala hii inahusu tofauti iliyopo baina ya vivumishi na vibainishi katika lugha ya Kiswahili. Tofauti hizo zinatokana na uainishaji wa aina za maneno hayo katika lugha ya Kiswahili kuonekana zikileta utata kutokana na sababu kuu tatu. Kwanza, ni kutokana na wanaisimu wengi wa Kiswahili kutokubaliana juu ya aina hizo za maneno kuwa ni tofauti. Pili, ni aina za maneno hayo kujidhihirisha katika mazingira sawa katika mpangilio wa maneno katika tungo tofauti. Tatu, ni kutokuwapo kwa vigezo vya uainishaji wa maneno hayo; yaani, vivumishi na vibainishi. Hivyo, makala hii imelenga kutengua mitazamo iliyozoeleka kuhusu dhana hizi na kubainisha kwa mifano tofauti zilizopo baina ya dhana hizi. Katika kufafanua tofauti hizo, makala hii imegawanyika katika sehemu kuu nne, nazo ni utangulizi, methodolojia, mjadala kuhusu tofauti hizo, na hitimisho.

## 1.1 Uainishaji wa Maneno

Uainishaji wa maneno ulianza katika kipindi cha Sarufi Mapokeo. Mwanaisimu wa Kigiriki, Dionysious Thrax alikuwa wa kwanza kuainisha maneno katika lugha ya Kigiriki. Dionysious Thrax (1874) alichambua aina kuu nane za maneno katika lugha nazo ni: nomino, kitenzi, kibainishi, kihusishi, kibadala (kiwakilishi), kielezi, kiungo (kiunganishi), na faridi pekee (neno lenye umbo na maana lakini

[1] Sehemu kubwa ya makala hii imetoka katika tasnifu yangu (2012).

haligawiki). Pamoja na kwamba katika uainishaji wake hakuwa na kivumishi, kibainishi kilikuwa kama aina mojawapo ya maneno (Khamis na Kiango, 2002). Katika lugha ya Kiswahili, wapo wanaisimu wengi walioainisha maneno kwa mtazamo huo wa kimapokeo. Mathalani, Nkwera (1978), Kapinga (1983), Mohamed (1986), Massamba, Kihore na Hokororo (1999), na Kihore, Massamba na Msanjila (2007) wanaeleza kuhusu kuwapo kwa aina saba za maneno ya Kiswahili; nazo ni: nomino/majina, kitenzi, kivumishi, kiingizi, kiwakilishi, kielezi, na kiunganishi/kihusishi. Kwa upande mwingine, Mdee (1988), Msokile (1992), Mbaabu (1992), Mgullu (1999), na Rubanza (2003) wameainisha aina nane za maneno ya Kiswahili. Aina hizo ni: nomino, kitenzi, kivumishi, kiwakilishi, kielezi, kiunganishi, kihusishi, na kiingizi. Pamoja na kutofautiana kwa idadi ya aina za maneno, wanaisimu wa makundi yote mawili, katika uainishaji wao, hawakuonyesha *kibainishi* kama aina mojawapo ya maneno katika lugha ya Kiswahili.

Zaidi ya hao, Habwe na Karanja (2004:131) wameainisha aina kumi za maneno katika Kiswahili. Nazo ni nomino, kitenzi, kivumishi, kiwakilishi, kielezi, kiunganishi, kihusishi, kihisishi, kionyeshi, na kibainishi. Licha ya kuainisha kibainishi kama aina mojawapo ya maneno, wanaisimu hawa wanasema kuwa aina hii haimo katika lugha ya Kiswahili. Wanashadidia kwa kudai kwamba kuna lugha zilizo na vibainishi lakini siyo lugha ya Kiswahili. Wanasema, mathalani, katika lugha ya Kiingereza kuna vibainishio (*articles*) kama vile "*a*", "*an*", na "*the*", ambavyo hutumika pamoja na nomino. Ukichunguza maelezo ya wanaisimu hawa, utaona kuwa wanaelekea kutaja aina moja tu ya vibainishi kati ya aina tano zilizoainishwa na Richards na Schmidt (2002: 152), ambazo ni:

i) vibainishi vibainishio (havipo katika lugha ya Kiswahili);
ii) vibainishi vionyeshi, mfano: *hiki*, *huyu*, *yule*, *hii*, n.k;
iii) vibainishi vimilikishi, mfano: *yangu*, *yake*, *yako*, *yao*, *yetu* n.k; na
iv) vibainishi kiasi, mfano: *yote, wote*, *yoyote*, *wowote*, *wengine*, *mengi*, *vingi* n.k; na
v) vibainishi namba, mfano: *mmoja*, *wawili*, *wanne* n.k.

Habwe na Karanja (wameshatajwa) wanataka kutuaminisha kuwa kukosekana kwa aina ya kwanza ya vibainishi (yaani vibainishio) katika Kiswahili kunasababisha kutokuwapo kwa kategoria nzima ya kibainishi katika lugha hii. Madai hayo si ya kweli, kwa sababu kuna aina nyinginezo za vibainishi katika lugha ya Kiswahili, kama tutakavyoona katika makala hii. Licha ya kuwapo kwa vibainishi vya aina nyinginezo katika lugha hii, vibainishi hivyo huwekwa katika kategoria ya vivumishi. Makala hii inaona kwamba kibainishi ni kategoria mojawapo ya aina za maneno ya Kiswahili.

### 1.2 Dhana ya Kivumishi na Kibainishi

Dhana ya *kivumishi* na *kibainishi* si ngeni sana katika uwanja wa isimu hususani katika sintaksia. Uchunguzi wa kiisimu unaonyesha kuwa katika kipindi cha Sarufi Mapokeo (tangu karne ya tatu Kabla ya Kristo enzi za Sarufi ya lugha ya Kilatini na Kigiriki), dhana ya *kivumishi* ilitumiwa kumaanisha neno linalokumusha (yaani, neno linalotoa taarifa zaidi kuhusu) nomino. Baadhi ya wanaisimu wa lugha ya Kiswahili wanaofasili dhana ya kivumishi kwa mtazamo wa Sarufi Mapokeo ni Kapinga (1983:15), Mohamed (1986:6), TUKI (1990:40), Rubanza (1996), Massamba na wenzake (1999) na Kihore na wenzake (2007). Kwa upande mwingine, dhana ya kibainishi ilianza kutumika katika karne ya 20 hasa baada ya kuasisiwa kwa Sarufi Geuzi Zalishi na Noam Chomsky (1965). Wanasarufi Geuzi Zalishi waliona kuwa kulikuwa na haja ya kuwa na dhana ya kibainishi kama aina mojawapo ya maneno iliyo tofauti na dhana ya kivumishi. Mathalani, Richards na Schmidt (2002:152) wanafasili kuwa kibainishi ni neno linaloambatana na nomino, nalo huonyesha ukomo wa maana ya nomino kwa kiasi fulani.

Licha ya Wanasarufi Geuzi Zalishi kuingiza dhana ya kibainishi kutumika kama aina mojawapo ya maneno, dhana hii imekuwa ni tatizo katika lugha ya Kiswahili, yaani kumekuwa na tatizo la kuainisha vibainishi katika lugha ya Kiswahili. Kama tulivyodokeza awali, inaelekea kuwa hakuna mwanaisimu yeyote aliyewahi kuviainisha vibainishi kama aina mojawapo ya maneno ya Kiswahili. Badala yake, wanaisimu wengi wa lugha hii wamekuwa wakiichanganya dhana hii ya kibainishi na kivumishi, yaani aina za vibainishi kuainishwa kama aina za vivumishi. Uainishaji uliofanywa na wanaisimu mbalimbali katika lugha ya Kiswahili kuhusu aina za maneno, kwa kuchanganya kategoria ya vivumishi na vibainishi katika kapu moja unaibua maswali mengi yanayohitaji majibu. Je, kibainishi ni nini? Je, kibainishi hutofautiana na kivumishi? Kwa lugha zinazotajwa kuwa na vibainishi na vivumishi, wanaisimu wametumia vigezo vipi kutofautisha dhana hizi mbili? Kama vibainishi hutofautiana na vivumishi, je kuna vibainishi katika lugha ya Kiswahili? Je, tofauti ya vibainishi na vivumishi hudhihirikaje katika Kiswahili? Tunaamini kwamba maswali haya yanatosha kuona kuwa kuna utata unaohitaji kutatuliwa ili kuweza kutofautisha dhana hizi katika Kiswahili.

### 1.3 Uainishaji wa Vivumishi vya Kiswahili Kimapokeo

Pamoja na wanaisimu wa Kiswahili kukubaliana kuhusu kuwapo kwa dhana ya kivumishi katika lugha hii, mitazamo yao inatofautiana kuhusu uainishaji wa vivumishi hivyo. Wapo wanaosema lugha hii ina aina tano za vivumishi nazo ni: (i) vivumishi vya sifa, (ii) vivumishi vimilikishi, (iii) vivumishi vya idadi, (iv) vivumishi vionyeshi, na (v) vivumishi viulizi (Kihore na wenz. 2007; Besha, 2007). Pamoja na aina hizo tano za vivumishi katika Kiswahili, Mohamed

(2001:66-68) anadai kuwapo kwa aina nyingine ya sita, anayoiita vivumishi vya a-unganifu.

Kwa upande wake, Rubanza (2003:72-75) anasema kuwa kivumishi ni kipashio kitoacho habari zaidi kuhusu nomino. Anasema katika lugha ya Kiswahili kuna aina tatu tu za vivumishi, nazo ni:

(i) vivumishi vya sifa, kwa mfano: -ema, -dogo, -vivu, -geni, stadi, nadhifu, bora n.k;
(ii) vivumishi vya idadi, kwa mfano: watoto *wawili*, wafanyakazi *wengi*, mti *mmoja*; na
(iii) vivumishi vya pekee, kwa mfano: *ingine*, *-ote*, na *-o--ote* kama katika maneno *mwingine*, *wote*, na *chochote*.

Hata hivyo, Rubanza anahitimisha kuwa katika mtazamo wa Nadharia ya Sarufi Geuzi Zalishi maneno aliyoyapa sifa ya uvumishi na uwakilishi kwa mpigo kwa mfano: *hili*, *haya*, *yale*, *huyu*, *huyo*, *yule*, *yangu*, *yetu*, *yako*, *yenu*, *yake*, *yao* huitwa *vibainishi*, ambavyo ni *vikumushi* (*modifiers*). Vikumushi hivi vina uwezo wa kukumusha nomino na hata kushika nafasi ya nomino (kama alivyotaja hapo awali) iwapo nomino inadondoshwa katika muktadha maalumu. Pamoja na kuonyesha mtazamo wa Nadharia Sarufi Geuzi kuhusu dhana ya kibainishi, hajaonesha kuwa msimamo wake ni upi juu ya maneno hayo; Je, bado ni vivumishi au viwakilishi ama vibainishi?

Nao, Khamisi na Kiango (2002:56-58) wanasema kuwa vivumishi ni maneno ambayo hukumusha (yaani, huongeza sifa au taarifa muhimu) nomino. Wanaendelea kushadidia kwa kusema kuwa kivumishi ni neno linalofanya nomino ivume. Wao wanaainisha aina mbili za vivumishi, ambazo ni:

i) vivumishi vya sifa, mfano: *mzuri*, *mbaya*, *mnene*, *mfupi*;
ii) vivumishi vya idadi, mfano: *mchache*, *chote*.

Naye, Mgullu (1999: 157) anasema kivumishi ni neno ambalo hueleza zaidi juu ya nomino. Anaainisha aina sita za vivumishi, yaani:

(i) vivumishi vya sifa; mfano: *safi*, *nzuri*, *dhaifu*, *mrefu*, *mweusi* n.k;
(ii) vivumishi vimilikishi; mfano: *–angu*, *-etu*, *-ako*, *-enu*, *-ake*, *-ao*;
(iii) vivumishi vionyeshi; mfano: *huyu*, *huyo*, *yule*, n.k;
(iv) vivumishi vya idadi; mfano: *mbili*, *watatu*, *wote*, *nyingi*, *ndogo*;
(v) vivumishi viulizi; mfano: *ngapi*, *gani*, *-pi*; na
(vi) vivumishi visisitizi; mfano: *-enyewe*.

Kutokana na uainishaji huo, tumepata picha kuwa uainishaji wa kategoria ya vibainishi umekuwa ukichanganywa katika ‘kapu’ moja la vivumishi. Hivyo, uainishaji wa wanaisimu wa Kiswahili hapo juu umetusukuma kufanya mjadala wa kuonyesha tofauti ya dhana ‘kivumishi’ na ‘kibainishi’ katika lugha ya Kiswahili.

## 2.0 Methodolojia

Data nyingi za makala hii zimepatikana kutokana katika tasnifu yangu ya Umahiri iliyohusu "Changamoto Wazipatazo Wageni katika Kujifunza Kiswahili katika Taasisi za Elimu ya Juu: Uchunguzi Kifani wa Wanafunzi wa Kigeni Chuo Kikuu Dar- es Salaam (2012)". Mbinu ya udurusu wa tasinifu hii na mapitio ya maandiko mbalimbali ya wanaisimu wa lugha za kigeni na Kiswahili yamedhihirisha wazi tofauti kubwa baina ya vivumishi na vibainishi katika lugha ya Kiswahili. Tofauti hizo zilizobainishwa na udurusu huo ni fasili, sifa, na aina za vivumishi na vibainishi. Mbali na udurusu huo, baadhi ya kauli, sifa, na aina za vivumishi na vibainishi zimeakisi mawazo na maoni binafsi ya mwandishi wa makala hii na kamwe zisichanganywe na nukuu za mapitio ya maandiko. Aidha, orodha ya sifa na aina zilizobainishwa katika makala hii zinatoa vigezo vya msingi vya tofauti zilizopo baina ya vivumishi na vibainishi katika Kiswahili.

## 3.0 Mjadala kuhusu Tofauti ya Vibainishi na Vivumishi katika Lugha ya Kiswahili

Kutokana na dhana ya vibainishi kuingiliana na dhana ya vivumishi kisintaksia katika tungo, kuna haja ya kuchunguza upya uainishaji wa vibainishi na vivumishi katika lugha ya Kiswahili. Vibainishi vina tabia nyingi za kisemantiki na kisintakisia zinazosababisha kuwekwa katika kundi moja na vivumishi ambavyo vinaonekana kufanana sana katika nafasi za kisintakisia na kutafsiriwa kama kitu kimoja. Makala hii inapendekeza kwamba uainishaji wa dhana hizi uzingatie kigezo cha kisintaksia ili kuweza kuzitofautisha dhana hizi kimatumizi, yaani kuzingatia *mtawanyiko* wake, *dhima kisarufi*, na *mnyambuliko* wa aina hizi za maneno. Aidha, vipengele vinavyofuata hapa chini vimeainisha dhana ya vivumishi na vibainishi katika Kiswahili kwa mtazamo wa kisasa.

### 3.1 Uainishaji wa Vivumishi katika Lugha ya Kiswahili

Kivumishi ni neno linaloelezea kitu, tabia/ubora/jinsi (*quality*), hali, au tendo lililorejelewa na nomino (Richards na Schmidt, 2002:13; taz. pia Mohamed, 2001:63; Habwe na Karanja, 2004; na Mgullu, 2002). Kivumishi ni neno ambalo hukumusha (yaani, huongeza sifa au taarifa muhimu) nomino. Khamisi na Kiango (2002) wanasema kuwa neno hili huifanya nomino ivume, kwa mfano: *-nene*, *-pana*, *-refu*, *-fupi*, *-zuri*, *-baya*, *-kubwa*, *-dogo*, *-tamu*, *-chungu*, *-safi*, *-chafu*, *-embamba*. Khamisi na Kiango wanaeleza kuwa kimaumbile, vivumishi hudhihirika kwa namna mbili, yaani vivumishi vinavyochukua viambishi patanishi na vivumishi ambavyo havichukui viambishi patanishi.

Kuhusiana na vivumishi vinavyochukua viambishi patanishi, Khamisi na Kiango (2002) wanasema kwamba hivi ni vivumishi vya asili vinavyotokana na lugha ya Kiswahili au lugha nyingine za Kibantu. Vivumishi hivi huchukua aina

mbalimbali za viambishi patanishi kulingana na ngeli ya nomino inayokumushwa, kwa mfano *-chafu*, *-dogo*, *-refu*, *-kubwa*, *-tamu*, *-chungu*. Vivumishi hivi hubadilika umbo kufuatana na ngeli ya nomino. Hii ni kutokana na tabia ya Kiswahili kujenga mfumo wa upatanisho wa kisarufi kati ya nomino na kivumishi. Jedwali namba 1 linaonyesha upatanisho huo katika lugha ya Kiswahili:

**Jedwali 1: Upatanisho wa Vivumishi kutokana na Ngeli za Nomino na katika Kiswahili**

| **Ngeli** | **Kiambishi cha Ngeli** | **Mfano** | **Kipatanisho cha Kivumishi** | **Mfano** |
|---|---|---|---|---|
| 1. | m | M-tu | m | m-refu |
| 2. | wa | Watu | wa | wa-refu |
| 3. | m | Mlango | m/w | m-pana |
| 4. | mi | Milango | mi | mi-pana |
| 5. | ji | Jiwe | ø/j | -dogo |
| 6. | ma | Mawe | ma | ma-dogo |
| 7. | ki | Kiti | ki | ki-bovu |
| 8. | vi | Viti | vi | vi-bovu |
| 9. | n | Ndoo | - | kubwa |
| 10. | n | Ndoo | - | kubwa |
| 11. | u | Uso | m | m-chafu |
| 12. | u | Nyuso | - | -chafu |
| 13. | u | Ufunguo | m | mfupi |
| 14. | ø | Funguo | - | -fupi |
| 15. | ku | Kusoma | ku | Ku-fupi |
| 16. | pa | Pa-hali | pa | Pa- embamba |
| 17. | mu | Mw-ahali | mu | Mu-andani |
| 18. | ku | Ku-hali | ku | Ku-embamba |

**Chanzo:** Philipo (2012)

Aina ya pili ya vivumishi ni ambayo haichukui viambishi patanishi, kwa mfano *hodari*, *zamani*, *maarufu*, *dhahiri*, *rahisi* na *safi*. Hata hivyo, idadi ya vivumishi vya aina hii si kubwa sana katika lugha ya Kiswahili. Vivumishi vingi vya aina hiyo ni vile vilivyoingizwa katika Kiswahili kutoka lugha za kigeni kama vile Kiarabu.

Naye, Mohammed (2001: 63) anasema kivumishi ni neno ambalo huelezea nomino ama kitu kuhusu ubora wake. Hivyo, tofauti na lugha nyingine kama vile Kiingereza, kivumishi katika lugha ya Kiswahili mara nyingi huwekwa mara baada ya nomino, yaani hufuata mara tu baada ya nomino ambayo huielezea. Pamoja na hilo, vivumishi hupokea viambishi awali. Viambishi hivi huambikwa kwenye mzizi wa kivumishi. Mfano (1) hapa chini unaonyesha viambishi hivyo:

(1) a) –refu **m-**refu
b) –nene **m**-nene

Pia, vivumishi hupokea ulinganisho katika tungo; katika Kiingereza kwa mfano, vivumishi huambatanisha viambishi ambavyo hubainisha ulinganifu. Viambishi hivyo ni *-er* na *-est* kama katika "*big, bigger, biggest*." Katika Kiswahili hakuna aina hiyo ya ulinganisho na badala yake hutumia maneno huru kama *kuliko, zaidi ya*, n.k. kama ilivyo katika mfuatano wa maneno katika mfano (2) hapa chini:

(2) a) nene *kuliko*...
b) nzito *zaidi kuliko*…
c) kubwa *kuliko*...
d) mrembo/mzuri *sana*.

Pamoja na wanaisimu hawa kuainisha aina za vivumishi kama tulivyoona hapo juu, tunaweza kuhitimisha kwamba kivumishi ni neno linalotoa taarifa za sifa/ tabia/jinsi/ubora/hali/kitaamuli (*qualitative*) katika kutafsiri nomino iliyoambatana nayo. Mathalani, mbuzi *mweupe*, mbuzi *mnene*, mbuzi *mkali*, mbuzi *mwepesi* n.k. Neno lolote ambalo hutoa taarifa zaidi kuhusu nomino huitwa kivumishi, na mara nyingi huja mara baada ya nomino kama vile mti *mrefu*, msichana *mrembo* n.k.

### 3.1.1 Sifa za Vivumishi katika Lugha ya Kiswahili

Vivumishi vyote vina sifa ya kileksika na kimaudhui, yaani hutokana na kategoria ya kileksika ambayo kwa kawaida hubeba taarifa za maudhui ya kileksika. Maneno ya kileksika ni yale yenye maudhui ndani yake. Kwa mfano, vivumishi kama vile -*eusi*, *refu*, *-nene*, *-epesi* ni vivumishi vinavyoelezea maudhui ya kileksika kwa sababu vinaonyesha jinsi/hali yenyewe ilivyo. Kwa maana hiyo ni maelezo ya kimaudhui. Ili kujua neno kama lina maelezo ya kimaudhui ni kuangalia unyume (antonimu) wake; yaani, kama lina unyume basi neno hilo ni la kimaudhui. Mfano (3) unaonyesha kinyume kwa kila kivumishi:

(3) a) refu – fupi
b) zito – epesi
c) embamba – nene

Aidha, vivumishi vina sifa ya kupokea ulinganisho, yaani vivumishi hulinganishwa kwa kutumia vielezi. Mfano (4) unaonyesha ulinganisho huo:

(4) a) mtoto *mzuri* sana
b) mwanafunzi *hodari* kuliko
c) mchezaji *bora* zaidi

Sifa nyingine ni kwamba vivumishi kadhaa vinaweza kufuatana kuvumisha nomino moja. Mfano (5) unaonesha mfuatano huo wa vivumishi kadhaa kukumusha nomino:

(5) a) msichana *mrembo, mrefu, mnene*
b) kijana *hodari, mpole, mcheshi*
c) shati *nzuri, nyeupe, pana*

### 3.1.2 Aina za Vivumishi katika Lugha ya Kiswahili

Kutokana na fasili, sifa hizo, na mtazamo wa sasa tunaweza kuainisha aina saba (7) za vivumishi. Aina hizo pia zimeonyeshwa kwa muhtasari katika Jedwali (2):

1) vivumishi vya sifa/tabia, mfano: *mrembo, mtanashati, werevu, ukali, upole, maarufu, -baya, -zuri, hodari*;
2) vivumishi vya ukubwa/jinsi, mfano: *-dogo, -kubwa, -nene, -zito, -epesi, -pana, -fupi* ;
3) vivumishi vya umbo/hali, mfano: *mduara, mraba, mstatili*;
4) vivumishi vya wakati/umri, mfano: *-changa, -zee, -pya, zamani*;
5) vivumishi vya rangi, mfano: *bluu, nyeusi, nyeupe, kijani, nyekundu*;
6) vivumishi vya sabustansi/dutu, mfano: *plastiki, sufu, nailoni*, n.k;
7) vivumishi vya utaifa, mfano: *Mtanzania, Mchina, Mkenya, Mganda, n.k.*

**Jedwali 2: Uainishaji wa Vivumishi katika Kiswahili**

| **Utaifa** | **Sabustansi /dutu** | **Rangi** | **Umri/wakati** | **Umbo/Hali** | **Ukubwa/jinsi** | **Sifa/tabia** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mtanzania<br>Mchina<br>Mjapani<br>Mkenya<br>Mganda | plastiki<br>sufu<br>nailoni<br>pamba | bluu<br>nyeusi<br>nyeupe<br>kijani<br>nyekundu | -changa<br>-zee<br>-pya, zamani | mduara<br>mraba<br>mstatili<br>msonge<br>pembetatu | -dogo<br>-kubwa,<br>-nene<br>-zito<br>-epesi<br>-pana<br>-embamba<br>-fupi<br>-refu | mrembo<br>mtanashati<br>werevu<br>ukali upole<br>maarufu<br>-baya<br>-zuri,<br>chungu<br>tamu<br>safi |

Ufafanuzi wa aina hizo za vivumishi ni kama ifuatavyo:

### (i) Vivumishi vya Sifa/Tabia

Vivumishi vya sifa ni vivumishi vinavyotoa maelezo/taarifa ya maamuzi, hisia, msisitizo na tathmini. Mfano (6) unaonyesha vivumishi hivyo katika matumizi:

(6) a) mtu *mbaya*
b) msichana *mrembo*
c) mlango *bora*
d) kiti *kizuri*

Vivumishi hivyo ambavyo vipo katika hati mlazo vinaelezea hisia na tathmini katika kufanya maamuzi na kusisitiza juu ya nomino inayozungumziwa. Kwa

mfano, mtu anaposema “msichana *mrembo*” maana yake kuna hisia fulani zinazomwongoza mtu huyo kusema msichana huyu ni mrembo.

**(ii) Vivumishi vya Ukubwa/Jinsi**

Vivumishi vya ukubwa/jinsi ni vivumishi vinavyoelezea ukubwa au jinsi nomino ilivyo. Mfano (7) unaonyesha vivumishi hivyo na matumizi yake:

(7) a) mtu *mnene*
b) umbali *mrefu*
c) mzigo *mzito*

Vivumishi katika mfano (7) hapo juu vinaelezea jinsi au ukubwa wa nomino ulivyo.

**(iii) Vivumishi vya Umbo/Hali**

Vivumishi vya umbo/hali ni vile vinavyoonyesha umbo au hali ya nomino inayoelezewa na kivumishi hicho kama mfano (8) unavyoonyesha:

(8) a) nyumba *mduara*
b) umbo *mraba*
c) kitabu *mstatili*

9) a) nyumba *ya msonge*
b) meza *ya duara*
c) umbo *la mraba*

Katika Kiswahili aina hii ya vivumishi huhitaji kiunganishi cha a-unganifu ili kiweze kueleweka kwa watu kama inavyoonyeshwa katika mfano (9) hapo juu. Pia, pamoja na vivumishi hivyo kuhitaji viunganishi vya a-unganifu, ikumbukwe kuwa mfano (8) unaweza kutumika katika tungo za Kiswahili na kueleweka kwa wazungumzaji wa Kiswahili.

**(iv) Vivumishi vya Wakati/Umri**

Vivumishi vya wakati/umri ni vivumishi vinavyoelezea wakati au umri wa nomino husika kama mfano (10) unavyoonyesha:

(10) a) mtoto *mchanga*
b) mwaka *mpya*
c) mtu *mzima*

**(v) Vivumishi vya Rangi**

Vivumishi vya rangi ni vile vinavyoelezea rangi ya nomino. Rangi katika lugha ya Kiswahili huainishwa katika aina mbili: rangi za msingi (nyeusi, nyeupe, na nyekundu), na rangi zisizo za msingi (bluu, kijani, njano, kahawia, n.k). Kimsingi, aina za rangi katika lugha nyingi za Kibantu ni tatu tu (yaani nyeusi, nyeupe, na nyekundu). Mfano (11) unaonyesha vivumishi vya rangi:

(11) a) kalamu *nyeusi*
b) karatasi *nyeupe*
c) nguo *nyekundu*

(12) a) kalamu *ya bluu*
b) karatasi *ya njano*
c) tai *ya kijani*

Aina nyingine za rangi ambazo hazipo katika lugha za Kibantu zimetokana na lugha za kigeni. Hivyo, rangi hizi zinapoingia katika lugha ya Kiswahili huhitajia kiunganishi cha a-unganifu ili ziweze kueleweka kwa watu, kama mfano (12) unavyoonyesha.

**(vi) Vivumishi vya Substansi/Dutu**

Vivumishi vya subustansi/dutu huelezea jinsi nomino ilivyoundwa; mfano (13) unaonyesha vivumishi hivyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| (13) | a) *nguo *pamba* | (14) | a) nguo *ya pamba* |
| | b) *mfuko *nailoni* | | b) mfuko *wa nailoni* |
| | c) *ndoo *plastiki* | | c) ndoo *ya plastiki* |

Katika Kiswahili vivumishi hivi huhitaji viunganishi vya a-unganifu ili viweze kueleweka kwa watu kama inavyoonyeshwa katika mfano (14) hapo juu. Mfano (13) si sahihi katika tungo za Kiswahili kutokana na kwamba havina viunganishi vya a-unganifu. Hivyo, vivumishi hivyo vikitumika kuelezea nomino hizo, zinaweza zikaleta utata au zisieleweke kwa wazungumzaji wa Kiswahili.

**(vii) Vivumishi vya Utaifa**

Vivumishi vya utaifa ni vivumishi vinavyoonyesha utaifa wa nomino inayoelezewa. Yaani, utaifa huvumisha nomino iliyotangulia katika tungo; mfano (15) unaonyesha vivumishi hivyo:

(15) a) mwanafunzi *Mtanzania*
b) mwalimu *Mkenya*
c) mhandisi *Mchina*

Kipengele hiki kimeonyesha uainishaji wa vivumishi katika lugha ya Kiswahili. Kipengele kinachofuata kinaainisha vibainishi katika lugha ya Kiswahili.

### 3.2 Uainishaji wa Vibainishi katika Lugha ya Kiswahili

Kibainishi ni neno ambalo hutumika pamoja na nomino nalo kwa kiasi fulani huweza kuonyesha ukomo wa maana ya nomino (Richards na Schmidt, 2002: 152). Kibainishi hufafanua kitu kiidadi (*quantitative*) ama kutambulisha tafsiri ya nomino, mfano: mbuzi *wengi*, mbuzi *wachache*, mbuzi *huyu*, mbuzi *hawa* n.k. Vibainishi ni maneno yenye dhima ya kisarufi yanayotumika kuonyesha aina ya kirejelewa ambayo nomino hiyo inayo.

#### 3.2.1 Sifa za Vibainishi katika Lugha ya Kiswahili

Vibainishi vyote vina sifa ya kisarufi, yaani hubeba taarifa za kisarufi ambazo huonyesha idadi, nafsi, uhusika, ngeli, dhamira, na jinsi (Radford, 2004:34). Vibainishi havina taarifa za kimaudhui, yaani huwezi ukachora picha ya nafsi,

idadi n.k. Vibainishi, hubainisha seti ya sifa za kisarufi tu kama tulivyozitaja. Mifano ya 16, 17 na 18 inaonyesha sifa za kisarufi za vibainishi hivyo:

| **Idadi** | **Nafsi** | **Ngeli** |
|---|---|---|
| (16) a) watoto *wawili*<br>b) wanafunzi *wote*<br>c) kalamu *kumi* | (17) a) kitabu *changu*<br>b) nyumba *yake*<br>c) mtoto *wetu* | (18) a) kitabu *hiki*<br>b) nyumba *hii*<br>c) mtoto *huyu* |

Mifano ya 16, 17, na 18 inaonyesha taarifa za kisarufi tu. Mathalani, tukisema "watoto *wawili,*" hapa kibainishi "*wawili*" hakivumishi nomino bali kinabainisha idadi ya nomino "watoto." Kibainishi "*wawili*" kimefanya kazi ya kisarufi ambayo ni kuonyesha idadi. Idadi hiyo ndiyo inayobainisha kuwa kuna "watoto wawili". Tukisema "kitabu *changu*" hapa kibainishi "*changu*" hakivumishi nomino bali kinabainisha umiliki wa nomino "kitabu". Kibainishi "*changu*" kimefanya kazi ya kisarufi ambayo ni kuonyesha nafsi ya umiliki. Kwa kifupi, vibainishi hubainisha nomino na vivumishi huvumisha nomino na kuifanya nomino hiyo ivume kitabia/sifa/kiubora/kihali.

Sifa nyingine ya vibainishi ni kwamba havina sifa ya kupokea ulinganisho katika tungo, yaani huwezi ukaongezea neno jingine; vinafunga mlango wa kuendelea kufafanua juu ya nomino hiyo. Hoja hii ni kwa vibainishi tu kama vile 'wangu', 'wawili' na 'hii' na si kwa maneno mengine. Maneno kama vile 'mzuri', wachanga' na 'ndogo' hayo ni vivumishi ndiyo maana yanakubali kupokea ulinganisho wa maneno kama vile 'sana' na 'kuliko'. Tunachosisitiza hapa ni kwamba katika tungo zifuatazo huwezi ukaongezea neno jingine lenye kuonyesha ulinganisho (kama vile 'sana' na 'kuliko'). Mfano (19) unaonyesha sifa hiyo:

(19) a) * mtoto *wangu* sana
b) *watoto *wawili* sana
c) *gari *hii* kuliko

Mfano (19) unapingana na tungo za Kiswahili kwani katika hali ya kawaida mtu hasemi tungo kama hizo. Hii ni kuukilia ukweli kwamba kazi ya kibainishi ni kubainisha tu na si kuvumisha nomino, yaani kutoa maelezo ya ziada. Kwa mfano, ingekuwa ni kivumishi tungeweza kuwa na tungo kama hizi zinavyoonekana katika mfano (20):

(20) a) watoto *wazuri* sana
b) gari *nzuri* kuliko
c) mwanafuzi *bora* zaidi

Sifa nyingine ni kwamba vibainishi huzingatia kanuni maalum ya mpangilio wa maneno katika tungo ili kukumusha nomino moja, yaani huwezi ukawa na kibainishi kinachofuata kibainishi kingine bila kufuata kanuni maalum. Inaelezwa na wanazuoni kama vile Rugemarila (2007), Mwihaki (2007), na Lusekelo (2009)

kuwa mpangilio wa vibainishi katika lugha za Kibantu hususani Kiswahili katika tungo huanza na vibainishi vimilikishi na kufuatiwa na vibainishi vionyeshi. Kutokana na sifa hiyo, Rugemarila (2007:137) anadokeza kuwa katika Kiswahili inawezekana kufuatana vibainishi vya aina mbili, yaani vimilikishi na vionyeshi tu. Hivyo, kuna kanuni ya kufuatana kwa vibainishi, yaani kibainishi kinachofuatia baada ya nomino ni kimilikishi na kufuatiwa na kionyeshi, kama inavyoonekana katika mfano (21). Pia, mfano (22) unaonyesha jinsi vibainishi visivyoweza kufuatana baada ya nomino:

| | | | |
|---|---|---|---|
| (21) | a) kitabu *changu kile* | (22) | a) *nyumba *hii yangu nyingine* |
| | b) watu *wangu hawa* | | b) *Shule *mbili hizi zozote* |
| | c) mti *wangu huu* | | c) * mtoto *mmoja yeyote* |

Aidha, Rugemarila (keshatajwa) anaendelea kudai kuwa ili kutatua tatizo la vibainishi hivi (yaani vimilikishi na vionyeshi) kushindania nafasi, Kiswahili kinaruhusu pia vionyeshi kukaa mwanzoni mwa nomino. Mfano (24) unaonyesha ukweli huo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| (23) | a) **mtu** *wangu yule* | (24) | a) *yule* **mtu** *wangu* |
| | b) **kitabu** *changu kile* | | b) *kile* **kitabu** *changu* |
| | c) **watu** *wangu hawa wote* | | c) *hawa* **watu** *wangu wote* |
| | d) **mti** *wangu huu* | | d) *huu* **mti** *wangu* |

Sifa ya mpangilio wenye kanuni maalum ya maneno katika tungo ili kukumusha nomino moja, hatutegemei kuikuta katika vivumishi kwani katika vivumishi tungeweza kuwa na tungo kama zinavyoonekana katika mfano (25):

(25) a) **mrefu* **msichana** *mrembo, mnene*
b) **mpole* **kijana** *hodari, mcheshi*
c) **nyeupe* **shati** *nzuri, pana*

Ingawa tungo hizi si sawa kwa upande wa vivumishi, pia kwa vibainishi si mpangilio kubalifu wa tungo za Kiswahili bali huweza kutokea katika tungo za lugha ya maongezi ya kawaida ya wazungumzaji wa Kiswahili.

Sifa nyingine ya vibainishi ni kutangulia kivumishi katika tungo na si kivumishi kutangulia kibainishi. Mfano (26) unaonyesha kanuni hiyo na mfano (27) unaonyesha ukiukwaji wa kanuni hiyo katika lugha ya Kiswahili:

| | | | |
|---|---|---|---|
| (26) | a) kitabu *hiki* kizuri | (27) | *a) kitabu kizuri *hiki* |
| | b) kijana *huyu* mtanashati | | *b) kijana mtanashati *huyu* |
| | c) wanafunzi *wawili* warefu | | *c) wanafunzi warefu *wawili* |

Katika kuhitimisha sehemu hii ni vema kusisitiza kwamba vibainishi haviruhusu upokeaji wa neno jingine lenye kuonyesha ulinganisho (kama vile ‘sana’ na

'kuliko'), bali vinaweza kuongeza maneno mengine tu ambayo hayaonyeshi ulinganisho.

### 3.2.2 Aina za Vibainishi katika Lugha ya Kiswahili

Makala hii imebainisha kuwa aina za vibainishi katika lugha ya Kiswahili ni kama ifuatavyo (pia taz. Richards na Schmidt, 2002: 152 ambao walibainisha katika lugha ya Kiingereza):

i) vibainishi vionyeshi, mfano: *hiki*, *huyu*, *yule*, *hii*;
ii) vibainishi vimilikishi, mfano: *yangu*, *yake*, *yako*, *yao yetu*;
iii) vibainishi vya kiasi, mfano: *yote*, *yeyote*, *wowote nyingine*, *wengine*, *mengi*, *vingi*; na
iv) vibainishi vya namba/idadi, mfano: *mmoja*, *wawili*, *wanne*.

Ni muhimu kuzingatia kwamba wakati mwingine aina za vibainishi huweza kuonekana zinafanana na aina za viwakilishi. Kimsingi, aina za vibainishi ni tofauti na aina za viwakilishi. Hii ni kwa sababu viwakilishi vinakosa maudhui ya kirejelewa yanayotolewa na nomino. Hivyo, viwakilishi hutegemea zaidi muktadha katika kutafsiriwa. Ilhali, vibainishi huonyesha kirejelewa kinachotolewa na nomino, na kwa hiyo hakuna kutegemea muktadha katika kutafsiri. Kwa mfano:

| Aina ya Vibainishi | Aina ya Viwakilishi |
|---|---|
| **Vibainishi vionyeshi**: *hiki, huyu, yule, hii*<br>Huonyesha kirejelewa kama kipo karibu au mbali kutoka kwa mnenaji. Pia, huonyesha kirejelewa kama ni umoja ama wingi. Mfano: mwanangu *yule* | **Viwakilishi vionyeshi**: *hiki, huyu, yule, hii*<br>Hutofautisha kirejelewa cha karibu na kirejelewa cha mbali. Pia, hutofautisha umoja na wingi wa nomino.<br>Mfano: *Yule* ni mwanangu |
| **Vibainishi vimilikishi**: *yangu, yake, yako*<br>Huonyesha kirai nomino kwa kuhusianisha na mnenaji/mwandishi. Hufanya nomino kuwa mahsusi. Mfano: Nyumba *yetu* | **Viwakilishi vimilikishi**: *yangu, yake, yako*<br>Hutokea mwanzoni mwa tungo. Hivyo, hutegemea muktadha zaidi.<br>Mfano: *Yetu* ni nzuri |

**Chanzo**: Biber na wenzake (2005)

Baada ya ufafanuzi huo mfupi baina ya vibainishi na viwakilishi, sehemu inayofuata inatoa ufafanuzi wa aina za vibainishi kama ambavyo tumevitaja hapo awali.

### i) Vibainishi Vionyeshi

Kionyeshi ni neno ambalo hurejelea mtu/kitu katika hali ya kuwa katika ukaribu ama umbali kutoka kwa mnenaji (Richards na Schmidt, 2002: 148). Maneno hayo husaidia kutofautisha kiasi cha ukaribu wa kirejelewa/kitajwa cha nomino kwa msemaji na/ama mrejelewa. Hivyo, vionyeshi huonyesha ukaribu wa kitajwa cha nomino kuu katika kirai nomino kuhusiana na mnenaji, mrejelewa ama wote.

Katika Kiswahili, vionyeshi huweza kutofautishwa kwa namna nyingi. Mzizi **h-** hutumika kuonesha ukaribu na mzizi **-le** huonesha umbali (Mohammed, 2001:172). Mohammed (2001:172) anasema kwamba vipengele hivi vya kisarufi hutumika katika muktadha ambapo ukaribu na umbali wa mahali ama muda vimependekezwa. Aidha, Ashton (1982) anafafanua kuwa wakati mzizi unapokuwa **h-o,** suala la ukaribu ama umbali linakuwa halipo kwa sababu kwa kawaida huonesha kitu kilichotajwa awali. Pia, Polome (1967) anaamini kwamba mzizi **h-** na **-le** huashiria "ukaribu ama umbali katika muda na nafasi" mtawalia, na katika **h-o**, Polome (1967) anasema kuwa mzizi unaonesha kitu kilichokwishatajwa. Wanaisimu wengine, kama vile Perott (1951), Wilson (1970), Zawawi (1971) na Kapinga (1983) wanataja mahali tu na hawarejelei suala la muda. Aidha, Longman (1965) anaonesha **h-** kama '*this*' na **-le** kama '*that*' na hajaonesha maelezo ya wazi juu ya ukaribu au umbali. Mfano (28) unaonyesha mizizi ya vionyeshi hivyo:

(28)
a) mtu *h+u+yu* = mtu *huyu*
b) mtu *h+u+yo* = mtu *huyo*
c) mtu *y+u+le* = mtu *yule*

Kutokana na maelezo hapo juu, aina tatu za vibainishi vionyeshi zinaweza kubainishwa katika lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo, vibainishi vionyeshi katika lugha ya Kiswahili hutumika katika namna tatu ambazo ni:

i) vionyeshi vya kawaida vya ukaribu ambavyo huonesha kirejelewa cha karibu kwa msemaji; mfano: (a) mtoto *huyu,* b) mti *huu,* (c) nyumba *hii*
ii) vionyeshi vya ukaribu ambavyo huonesha kirejelewa ambacho kipo karibu na mrejelewa; mfano: (a) mtoto *huyo,* (b) mti *huo,* (c) kitabu *hicho*
iii) vionyeshi vya umbali ambavyo huonyesha kirejelewa ambacho kipo mbali kwa wote, yaani msemaji na muonyeshwaji. Pia, hutumika kwa malengo ya kurejelea; mfano: (a) mtoto *yule*, (b) mti *ule,* (c) kitabu *kile*.

Jedwali (3) linaonyesha aina za vibainishi vionyeshi katika lugha ya Kiswahili:

**Jedwali 3: Vibainishi Vionyeshi Kutokana na Ngeli za Nomino katika Kiswahili**

| Ngeli | Kiambishi cha Ngeli | Mfano | Vibainishi Vioneshi | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Karibu | Mbali 1 | Mbali 2 (zaidi) |
| 1 | m | Mtu | huyu | huyo | yule |
| 2 | wa | Watu | hawa | hao | wale |
| 3 | m | Mlango | huu | huo | ule |
| 4 | mi | Milango | hii | hiyo | ile |
| 5 | ji | Jiwe | hili | hilo | lile |
| 6 | ma | Mawe | haya | hayo | yale |
| 7 | ki | Kiti | hiki | hicho | kile |
| 8 | vi | Viti | hivi | hivyo | vile |
| 9 | n | Ndoo | hii | hiyo | ile |
| 10 | n | Ndoo | hizi | hizo | zile |
| 11 | u | Uso | huu | huo | ule |
| 12 | n | Nyuso | hizi | hizo | zile |
| 13 | u | Ufunguo | huu | huo | ule |
| 14 | ø | Funguo | hizi | hizo | zile |
| 15 | ku | Kusoma | huku | huko | kule |
| 16 | pa | Pa-hali | hapa | hapo | pale |
| 17 | mu | Mw-ahali | humu | humo | mle |
| 18 | ku | Ku-hali | huku | huko | kule |

**Chanzo:** Philipo (2012)

### ii) Vibainishi vya Kiasi/ Wingi

Kibainishi cha wingi/kiasi (quantifier) ni neno ama kirai ambacho hufanya kazi pamoja na nomino na huonyesha wingi ama kiasi (Richards and Schmidt, 2002: 436). Katika Kiswahili, mzizi wa vibainishi vya kiasi ni -te, na -o-o-te pamoja na -ingi, na –ingine. Jedwali (4) linaonyesha aina za vibainishi vya kiasi/wingi kutokana na ngeli za nomino katika Kiswahili.

**Jedwali 4: Vibainishi vya Kiasi/wingi kutokana na Ngeli za Nomino katika Kiswahili**

| | | Vibainishi vya kiasi/wingi | | Vibainishi vya kiasi/wingi | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Ngeli** | **Kiambishi cha Ngeli** | **-ote** | **o-o-te** | **-ingi** | **-ingine** |
| 1 | m | - | yoyote | - | mwingine |
| 2 | wa | wote | wowote | wengi | wengine |
| 3 | m | wote | wowote | - | mwingine |
| 4 | mi | yote | yoyote | mingi | mingine |
| 5 | ji | lote | lolote | - | jingine |
| 6 | ma | yote | yoyote | mengi | mengine |
| 7 | ki | chote | chochote | - | kingine |
| 8 | vi | vyote | vyovyote | vingi | vingine |
| 9 | n | yote | yoyote | - | nyingine |
| 10 | n | zote | zozote | nyingi | zingine |
| 11 | u | wote | wowote | - | mwingine |
| 12 | n | zote | zozote | nyingi | zingine |
| 13 | u | wote | wowote | - | mwingine |
| 14 | ø | zote | zozote | nyingi | zingine |
| 15 | ku | kote | kokote | kwingi | kwingine |
| 16 | pa | pote | popote | pengi | pengine |
| 17 | mu | mote | momote | mwingi | mwingine |
| 18 | ku | kote | kokote | kwingi | kwingine |

**Chanzo:** Philipo (2012)

**iii) Vibainishi Vimilikishi**

Kimilikishi ni neno ama sehemu ya neno ambayo hutumika kuonyesha umiliki ama kumiliki (Richards na Schmidt, 2002: 408). Katika Kiingereza, kuna aina nyingi za vimilikishi, kwa mfano vibainishi vimilikishi, kama vile *my (*yangu*)*, *her* (yake), *your* (yako), *mine* (yangu), *hers* (yake), *yours* (yenu), n.k. Katika Kiswahili, mzizi wa kimilikishi mara nyingi huunganika na kisabiki chake (*its antecedent*), hutangulia mbele zaidi ya mizizi mingine na hutokea baada ya nomino. Jedwali (5) linaonyesha mizizi ya vibainishi vimilikishi vya nafsi:

**Jedwali 5: Mizizi ya Vibainishi Vimilikishi vya Nafsi**

| Nafsi | Mzizi wa Kimilikishi | Mfano |
|---|---|---|
| 1 Umoja | -angu | Mpira wangu |
| 2 Umoja | -ako | Mpira wako |
| 3 Umoja | -ake | Mpira wake |
| 1 Wingi | -etu | Mpira wetu |
| 2 Wingi | -enu | Mpira wenu |
| 3 Wingi | -ao | Mpira wao |

**Chanzo:** Philipo (2012)

### v) Vibainishi vya Namba/Idadi

Namba/idadi ni neno ambalo hutumika kuonyesha au kurejelea idadi ya nomino katika tungo. Hivyo, vibainishi vya idadi ni vibainishi vinavyoonyesha idadi ya nomino inayorejelewa. Katika Kiswahili, vibainishi vya idadi hufuata baada ya nomino, Jedwali (6) hapa chini linaonyesha vibainishi vya idadi/namba kutokana na ngeli za nomino katika Kiswahili:

**Jedwali 6: Vibainishi vya idadi/namba kutokana na Ngeli za Nomino katika Kiswahili**

| Ngeli | KNG | Mfano | Idadi/Namba | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | moja | mbili | tatu | nne | tano | sita | saba |
| 1 | m | M-tu | mmoja | | | | | | |
| 2 | wa | Watu | | wawili | watatu | wanne | watano | sita | saba |
| 3 | m | Mlango | mmoja | | | | | | |
| 4 | mi | Milango | | miwili | mitatu | minne | mitano | sita | saba |
| 5 | ji | Jiwe | moja | | | | | | |
| 6 | ma | Mawe | | mawili | matatu | manne | matano | sita | saba |
| 7 | ki | Kiti | kimoja | | | | | | |
| 8 | vi | Viti | | viwili | vitatu | vinne | vitano | sita | saba |
| 9 | n | Ndoo | moja | | | | | | |
| 10 | n | Ndoo | | mbili | tatu | nne | tano | sita | saba |
| 11 | u | Uso | mmoja | | | | | | |
| 12 | n | Nyuso | | mbili | tatu | nne | tano | sita | saba |
| 13 | u | Ufunguo | mmoja | | | | | | |
| 14 | ø | Funguo | | mbili | tatu | nne | tano | sita | saba |

**Chanzo:** Philipo (2012)

Hata hivyo, katika lugha ya Kiswahili vibainishi vya idadi hujidhihirisha kwa namna mbili. Kwanza, vile vinavyobeba viambishi (moja mbili, tatu, nne, na tano) kutegemeana na ngeli ya nomino. Aidha, kuna baadhi ya vibainishi vya idadi havina viambishi. Pili, visivyobeba viambishi (sita, saba, nane, tisa, na kumi) kama Jedwali 6 hapo juu linavyoonyesha.

## 4.0 Hitimisho

Makala imeonesha wazi kuwa maneno mengi yanayoitwa vivumishi yapo ambayo yanaweza kuainishwa kama vibainishi. Tatizo hili linatufanya tupate vivumishi vingi ambavyo tunashindwa kuviainisha chini ya msingi mmoja ulio thabiti na imara. Tatizo hili linajitokeza kwa sababu ya mazoea ya kuelewa dhana ya vivumishi. Katika kutatua tatizo hili, makala hii imetambua umuhimu wa tabia ya maneno katika tungo ya kuingiliana na kuathiriana kimaana na kikazi. Makala inapendekeza kutofautisha vivumishi na vibainishi kwa kutumia kigezo cha kisintaksia yaani: mfuatano wake katika tungo, mnyambuliko wake, na kazi zake kisarufi. Hii ndiyo misingi mitatu tunayotakiwa kuitumia kupambanua aina hizi za maneno, yaani kwa kuzingatia *mtawanyiko* wake, *dhima kisarufi*, na *mnyambuliko* wa aina hizi za maneno. Kwa kufanya hivyo tutakuwa tumeondoa kabisa utata wa kuviweka vibainishi katika 'kapu' moja la vivumishi.

## Marejeleo


Ashton, E.O. (1982). *Swahili Grammar (Including Intonation)*. London: Longman Green and Co. Ltd.

Besha, R.M. (2007). *Utangulizi wa Lugha na Isimu*. Dar-es-Salaam: DUP.

Biber, D, at el (2005). *Longman*: *Student Grammar of Spoken and Written English*. London Pearson Educational Limited.

Chomsky, N. (1965). *Aspect of the Theory of Syntax.* Cambridge: Massachusetts MIT Press.

Davidson, T. (1874). "Grammar of Dionysious Thrax". *Journal of Speculative Philosophy*. ST. Louis, Mo.

Habwe, J na P. Karanja (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*: Nairobi : Phoenix Publisher Ltd. Kapinga, M. C. (1983). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.

Khamis, A. M na J.G. Kiango (2002). *Uchanganuzi wa Sarufi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, TUKI.

Kihore Y.M, na Wenzake (2007). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu.* Dar es Salaam: TUKI. Longman, A. (1965). *Swahili Grammar and Syntax*. Pittsburgh: Duquesne University Press.

Lusekelo, A. (2009). "The Structure of the Nyakyusa Noun Phrase". Nordic Journal of African Studies 18 (4): 305 – 331.

Massamba, D.P.B, na Wenzake (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu.* Dar-es-

Salaam: TUKI.
Mbaabu, I. (1992). *Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Longman Kenya.
Mgullu, R.S. (1999). *Mtaala wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia, na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers (Kenya) Ltd.
Mgullu, R.S. (2002). *Mtaala wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia, na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers (Kenya) Ltd.
Mohamed, M. A. (1986). *Sarufi Mpya*. Dar-es-Salaam: Press and Publicity Center.
Mohamed, M. A. (2001), *Modern Swahili Grammar*. Nairobi: East African Educational Publishers.
Msokile, M. (1992). *Kunga za Fasihi na Lugha*. Dar es Salaam: Educational Publishers and Distributors Ltd.
Mwihaki, A. (2007). "A Minimalist Approach to Kiswahili Syntax". *Kiswahili* Journal of the Institute of Kiswahili Research 70: 17-140.
Nkwera, F. V. (1978). *Sarufi na Fasihi. Sekondari na Vyuo*. Mitaala ya lugha na Fasihi 4 Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
Perott, D. (1951). *Teach Yourself Swahili*. New York: David Mckay Company, Inc.
Polome, E.C. (1967). *Swahili Language Handbook*. Washington D.C: The center for Applied Linguistics.
Philipo, Z. (2012). Challenges Faced Foreigners while Learning Kiswahili in the Higher Learning Institutions. MA Dissertation of the University Dodoma.
Radford, A. (2004). *English Syntax: An introduction.* UK: Cambridge University Press.
Richards, J. C & Schmidt, R. (2002). *Longman Dictionary of Language Teaching and Applied Linguistics*: 3rd Edition, London: Pearson Education Limited.
Rubanza, Y.I. (1996). *Mofolojia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. TUKI
Rubanza, Y.I (2003). *Sarufi: Mtazamo wa Kimuundo*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
Rugemalira J. M (2007). "The Structure of the Bantu Noun Phrase". SOAS Working Papers in Linguistics Vol.15 pg. 135-148
TUKI, (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*: Dar es Salaam: Educational Publishers and Distributors Ltd.
Wilson, P. M. (1970). *Simplified Swahili*. Hong Kong: Longman Group (FE) Ltd.
Zawawi, S. (1971). *Kiswahili kwa Vitendo*. New York: Harper and Row.

**Vifupisho**

| | |
|---|---|
| **1, 2, 3 n.k ama NG** | Ngeli za Nomino |
| **KK** | Kipatanisho cha Kivumishi |
| **KNG** | Kiambishi cha Ngeli |
| **Na** | Namba |
| **UM** | Umoja |
| **WG** | Wingi |